BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Nane – Tarehe 24 Februari, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) ya Mwaka 2019/2020 na 2020/2021.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

85. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Wizara yetu ya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaundwa na vikosi mbali mbali vyenye majina tofauti na bila ya shaka kuna sababu tofauti za kuitwa kwa majina hayo, ikiwa ni pamoja na Kikosi cha Valantia.

(a) Kwa nini Kikosi kiitwe cha Valantia wakati ni jina la kiingereza na maana yake ni kujitolea, wakati watumishi wa kikosi hiki wanalipwa mishahara na malipo ya kustaafu kwao kama watumishi wengine wa Serikali.

(b) Je, hatuoni haja ya kubadilisha jina la kikosi hicho ili tuwe na jina linaloendana na mazingira yetu.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

140. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Katika jimbo la Dimani vipo viwanja vikubwa vya mchezo wa mpira wa miguu vilivyopo Bweleo, Dimani, Maungani na Nyamanzi. Viwanja vya Maungani vimekuwa vikitumika kwa mashindano ya ligi inayosimamiwa na ZFF. Hata hivyo, viwanja hivyo vipo katika hali mbaya na vinahitaji ukarabati wa miundombinu ikiwemo kuwekwa nyasi za bandia.

Je, Wizara ina mpango gani wa kusaidia kukiendeleza angalau kiwanja kimoja kati ya hivyo kwa kuweka miundombinu mizuri ikiwemo nyasi za bandia.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

163. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Naipongeza Serikali kwa kufanya juhudi za kuimarisha Uchumi wa Buluu hususani Sekta ya Uvuvi kwa kujenga masoko ya kisasa na madiko, kugawa boti za uvuvi na mengineyo. Hatua hizi zingeleta tija zaidi iwapo kungelikuwepo kiwanda cha kusarifu samaki kwa sababu kiwanda hicho ni kiungo muhimu cha kuongeza soko la samaki na vipato vya wavuvi wetu, lakini kiwanda hicho bado hakijajengwa hadi leo.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kukianzisha kiwanda hicho ili kiende sambamba na juhudi zake za kuimarisha Uchumi wa Buluu nchini.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

133. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Matamasha ya biashara nje ya nchi yana mchango mkubwa wa kuzitangaza bidhaa zetu kuweza kuingia kwenye soko la kimataifa.

(a) Je, ni kwa kiasi gani balozi zetu zinazotuwakilisha katika mataifa mbali mbali zinawajibika katika kuandaa matamasha haya.

(b) Ni faida gani zimepatikana kwa balozi zetu zinazoandaa matamasha ya biashara ya bidhaa za kitanzania.

(c) Ni bidhaa zipi katika maonesho hayo zimekuwa zikivutia soko la kimataifa hususan kwa wajasiriamali wadogo wadogo.

<u>Wizara ya Afya:</u>

42. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na changamoto nyingi kwa wasimamizi na watendaji wa hospitali katika kutoa huduma sahihi kwa wananchi kutokana na ufinyu wa bajeti.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kutoa huduma ya chakula na usafiri kwa kila hospitali hapa nchini.

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kupanga matumizi ya bajeti ya Wizara yako na ni vigezo gani huzingatiwa katika upangaji wa bajeti hiyo.

(c) Kwa kuwa suala la chakula cha wagonjwa limekuwa na changamoto na kupelekea kuwasumbua watendaji na wagonjwa, je, Wizara yako itaweka utaratibu gani wa kibajeti ili kuondoa usumbufu huo.

47. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Juhudi za Serikali katika vita dhidi ya maradhi sugu kama vile ukimwi, kifua kikuu na ukoma, zimeonesha kukosa nguvu katika siku za hivi karibuni.

(a) Je, Serikali ina mipango gani bora na iliyohakikiwa ya kudhibiti na kupambana na maradhi sugu Zanzibar.

(b) Je, kwa miaka 2020-2022, Serikali imetumia kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kutoa elimu juu ya maradhi sugu katika mashule, vyuo na taasisi nyengine za kielimu.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

63. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika awamu za awali za uongozi wa Serikali yetu, wanafunzi waliokuwa masomoni katika fani au mwelekeo wa fani mbali mbali, walifuatwa maskulini na vyuoni kwa ajili ya kuajiriwa, lakini hivi sasa wasomi na wahitimu wako wengi, huku ajira zimekuwa shida kupatikana.

Je, ongezeko la idadi ya watu lina mchango gani juu ya maboresho ya mtaala wetu kwenye sekta ya elimu katika suala zima la kuwaandaa wanafunzi wetu kuingia katika soko la ajira.

65. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tatizo la utoro wa wanafunzi hususan wakati wa masomo, linaathiri sana ufaulu wa wanafunzi wetu.

Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya tatizo hili kubwa hasa kwa skuli za Mwanakwerekwe na Magogoni.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

12. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni jambo la kimkakati kwa Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kutumia vyombo binafsi kusafirisha zana na vifaa vyake kutoka Unguja kwenda Pemba kwa kutumia meli na vyombo vyengine binafsi. Hata hivyo, kuna manung'uniko kwamba Serikali haijalipia baadhi ya huduma za meli za watu binafsi zilizosafirishia zana na vifaa vya Serikali kutoka Unguja kwenda Wesha Pemba.

(a) Je, kwa wastani, Serikali hugharamia kiasi gani inapokodi meli ya watu binafsi kutoka Unguja kwenda Wesha Pemba.

(b) Je, ni meli ngapi na zipi Serikali imekodi tokea mwaka 2010 na kiasi gani cha fedha kimelipwa na ambacho

hakijalipwa na lini kitalipwa.

(c) Je, ni ipi sababu ya Serikali kuchelewesha malipo ya kodi hizo za meli na kwa mwaka wa fedha 2022/2023 deni hilo limekusudiwa kulipwa kwa programu ipi.

44. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali imeendeleza jitihada za dhati za kujenga barabara za mijini na vijijini katika visiwa vya Unguja na Pemba. Hata hivyo, uwiano wa ubora na viwango vya barabara nyingi vimekuwa vikilalamikiwa.

(a) Je, Serikali inatumia chombo na utaratibu gani kukagua viwango vya barabara.

(b) Je, Serikali haioni ulazima wa kuimarisha kitengo maalumu cha kukagua viwango vya barabara (Zanzibar Road Inspection Unit – ZRIU) ili kusimamia na kuhakikisha ubora na ufanisi wa barabara.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

19. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Uwepo wa misitu katika mazingira yetu ni jambo muhimu sana kwani ni moja kati ya vianzio vya upatikanaji wa maji na mvua. Kwa vile iko miti mingi inayoendelea kupotea hapa nchini kama vile mibura na mianzi.

(a) Je, kwa kiwango gani Wizara inalijua jambo hili.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha miti hii inarejea kuwepo, ili kuzidi kuyalinda mazingira yetu.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

3. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na utaratibu wa mita za baadhi ya wateja kuwekwa juu kwenye nguzo za umeme zilizo karibu na wateja hao.

Je, ni sababu gani zinazopelekea kuwekwa mita hizo juu kwa

hivi sasa.

III. HOJA ZA KAMATI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) ya Mwaka 2019/2020 na 2020/2021.

Zanzibar,
24 Februari, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.